

Vyanzo vya Mitengo ya Wahusika Mashujaa katika Tungo za Kitendi za Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya-Tendi ya *Siri Sirini*

Neema Benson Sway na Shani Omari Mchepange
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Kifasihi, mitengo (umoja ‘mtengo’) inajumuisha kutengwa na kujitenga kwa wahusika mashujaa katika muktadha wa kisaikolojia, kiutendaji na kimazingira (Hegel, 1949; Seeman, 1959; Durkheim, 1964; Chiduo na wenzake, 2016). Utokeaji wake katika namna mbalimbali umefanya hata vyanzo vyake kuwa ni mahuluti, mintarafu ya tafiti zilizopo ambazo zimejikita zaidi katika mitengo ya kimazingira (Propp, 1968; Kunene, 1985; Senkoro, 1997; Michaux, 2003). Suala hili ndilo limechochea makala hii ambayo inachunguza vyanzo vya ujitokezaji wa mitengo mbalimbali ya wahusika mashujaa kupitia utungo wa *Siri Sirini*. Nadharia ya Mtengo na Mkabala wa Kitaamuli umetumika kuchanganua data za utafiti huu. Vyanzo vilivyobainika kusababisha mitengo ya wahusika mashujaa ni pamoja na suala la hofu ya kiongozi mkuu kwa shujaa, shujaa kutoridhishwa na utendaji wa kisiasa, mwito binafsi wa shujaa kitaifa, utangazi wa miiko ya kimila na shujaa kukwepa uhasama wa kiakraba. Makala imepanua maarifa kuhusu mambo yanayoibua mitengo ya wahusika mashujaa wa tungo za kitendi, kwani imefanikiwa kujumuisha vyanzo mbalimbali vinavyosababisha mitengo ya namna zote (ya kijiografia, kiutendaji na kisaikolojia) kwa ujumla wake. Matokeo yamepanua pia usafanuzi wa dhana hii ya mitengo katika fasihi na imetambulisha ufaafu wa nadharia ya ‘Mtengo’ katika uchambuzi wa kazi za kifasihi.

Maneno Muhimu: Mitengo, Wahusika Mashujaa, Tungo za Kitendi

Utangulizi

Mitengo ya wahusika mashujaa yaani kutengwa na kujitenga kwao kumesawiriwa kama kipengele cha kimotifu kwenye maisha ya wahusika mashujaa hasa wa tungo za kitendi (Rank, 1909; Campbell, 1956; Raglan, 1956; De Vries, 1963; Ansari, 2015). Mashujaa ni aina ya wahusika ambaa ndio uti wa mgongo wa utungo wowote wa kiutendi. Hawa ndio wanaobeba dhana nzima ya tungo za kitendi na maudhui ya msingi hususani ya kishujaa na kihistoria ya jamii au taifa fulani. Aidha, wahusika hawa hukutwa na mitengo mbalimbali wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao, hivyo ni kipengele muhimu kwenye ruwaza ya maisha yao. Tungo za kitendi ni kapu linalobeba aina tofauti za tungo zinazosawiri masuala ya msingi kuhusu jamii au taifa fulani kupitia matukio ya kishujaa na mashujaa kwa kutumia mitindo anuwai ya lugha. *Siri Sirini* inaingia kwenye tungo hizi za kitendi, kama riwayatendi inayotumia lugha ya mjazo ya kinathari yenye mawanda na uzito wa kiutendi (Mulokozi, 2017).

Mtengo ni dhana pana ambayo hujitokeza kwa namna mbalimbali kulingana na muktadha husika. Baadhi ya maandiko yanatoa maana ya jumla/ya kawaida ya dhana ya mtengo, ilhali wengine wameifafanua kimahususi zaidi. Baadhi ya maandiko yanaeleza kuwa, mtengo ni hali inayotokana na kitendo cha: “kuondosha, kutoa au kusababisha mwachano”, “watu au vitu viwili au zaidi kuwa mbali mbali”, “mtu kuwa mbali na jambo au wenzake” (Einblau, 1965; Sarfraz, 1997, TUKI, 2013; Shah, 2015; BAKITA, 2016; Chiduo na wenzake 2016). Kwa upande mmoja, suala la mwachano au kuwa mbali mbali linaweza kuwa la kijiografia baina ya wahusika, kwa maana ya mtu kuwa mbali na mahali pa pamoja. Hapa mitengo inarejelewa kama hali ya kuvuka mpaka fulani wa kieneo, yaani kitendo cha kutoka pahala fulani kwenda pengine kwa kuhusisha mwendo mrefu wa kisafari. Kwa upande mwagine, mwachano au umbali unaozungumziwa unarejelea pia suala la kukoma/kuondoshwa kwa mahusiano yaliyokuwapo au kutokea kwa mpaka wa kimahusiano na kimaigiliano baina ya pande mbili au zaidi zilizokuwa zikihusiana hapo awali (Einblau, 1965; Kaufmann, 1970;

Kanungo, 1982; Sarfraz, 1997; Shah, 2015). Hata hivyo, kisaikolojia na kiutendaji katika miktadha mbalimbali, mitengo ya wahusika imefafanuliwa kwa namna nyingine na wataalamu kama vile Rousseau (1947), Hegel (1949), Merton (1957) na Durkheim (1964). Mathalani, Rousseau (1947) na Hegel (1949) wanasesma, kisaikolojia mtengo hujitokeza pale mtu anapoamua kusalimisha au kuachana na masuala yake binafsi kama vile haki, uhuru, mamlaka, uwezo na malengo binafsi kwa ajili ya manufaa ya pamoja ya kijamii. Wataalamu hao (*weshatajwa*) wanaendelea kueleza kuwa, mtengo huu unapotokea mhusika huwa halazimishwi na mazingira; kwamba kwa hiari yake mwenyewe huamua kuachana na mambo yake binafsi na kuungana na wanajamii katika kufanya masuala ya kimajumui kwa manufaa ya pamoja. Aidha, Merton (1957) na Durkheim (1964) wanasesma, kiutendaji mtengo hutokeza pale mtu anapoamua kutokubaliana na mienendo na kaida zilizowekwa na jamii au kundi fulani. Wao wanasisitiza kuwa, mhusika huijengua au hujiweka mbali na kanuni zilizopo, yaani hujivua kwa kukiuka taratibu zilizopo, pale anapoona hazimnufaishi au kunufaisha wanajamii wanaomzunguka.

Kwa hiyo, ‘mtengo/mitengo’ ni kuwapo kwa mwachano au mpaka wa mahusiano na maingiliano ya kisaikolojia, kiutendaji na kijiografia baina ya mhusika mwenyewe au mhusika mmoja na wengine katika kazi ya kifasihi. Hata hivyo, pamoja na ujitokezaji mpana wa dhana ya mitengo, bado tafiti nyingi za kifasihi zimejiegemeza zaidi katika mitengo ya kijiografia, yaani ile ya safari za kimwendo. Kwa mfano, baadhi ya tafiti zimejikita katika kuchunguza sababu za mitengo ya safari za kimwendo (Kunene, 1985; Senkoro, 1997; Kemunto, 2015; Nyamsenda, 2015), ruwaza zake (Rank, 1909; Raglan, 1956; Campbell, 1956; De Vries, 1963), na tafiti nyingine zikieleza zaidi mitengo ya kijiografia kama tatizo linalowakumba wahusika wa kifasihi (Michaux, 2003; Ansari, 2015; Mwangi na wenzake, 2019). Kutokana na hayo, makala hii inaona ingelikuwa vyema vyanzo vyake pia vikajadiliwa kwa mapana yake, jambo ambalo limeshughulikiwa kupitia utungo teule wa kitendi wa *Siri Sirini*.

Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa katika kuupata utungo huo wa *Siri Sirini*, I-III (2013-2014). *Siri Sirini* iliteuliwa kwa kuwa ni mionganoni mwa utungo wa kiutendi (riwaya-tendi) wenye mhusika shujaa aliyeonekana kupitia mitengo mbalimbali katika ruwaza ya maisha yake. Kutokana na hilo, utafiti huu uliulenga moja kwa moja, kwa kuwa ulikuwa ni faafu kwa uchunguzi wa vyanzo vya ujitokezaji wa mitengo husika. Aidha, utafiti huu ni wa maktabani, hivyo mbinu ya usomaji makini wa sampuli teule (*Siri Sirini*) imetumika, na uchambuzi umefanywa kwa mkabala wa kitaamuli kutokana na kwamba, uchanganuzi wa data ulihuisha matini ya kiusimulizi.

Siri Sirini ni riwaya-tendi iliyotungwa na mwandishi Rocha M. Chimerah kutoka Kenya, yenye mfululizo wa majuzu matatu (3) kuanzia mwaka 2013 na 2014. Juzu la I, ni *Siri Sirini: Mshairi na Mfungwa* ambalo limetungwa mwaka 2013, mwaka 2014 likatungwa la II, *Siri Sirini: Mpiga Mbizi Kilindini* na la III, *Siri Sirini: Mtihani wa Mwanamke*. Ni mionganoni mwa utungo wa kiutendi uliosukwa kwa kuchota visa na historia za wahusika mashujaa wa kitendi, hususani wa tendi maarufu Afrika Mashariki ambazo ni *Mwanakupona*, *Fumo Liyongo* na *Sir L' asirar*. Aidha, umehusisha pia visa vya kidini hususani vya manabii na mitume na historia ya miji mikongwe ya Uswahilini, Afrika Mashariki. Kwa muhtasari, mkusanyiko wa majuzu haya unaelezea kuhusu maisha hasa ya kisiasa, kiutamaduni na kijamii ya watu wa taifa la Shanga ambalo mwandishi anasema ni mojawapo ya taifa la Barazinji. Maisha yao yanaelezwa kupitia kisa cha Mfalme Daudi Mringwari wa Abu, ambaye alikuwa ni mrithi wa Mfalme Malik Mringwari wa Abu, pamoja na ndugu yake mtoto wa shangazi aliyeitwa Fumo Liyongo ambaye ndiye alikuwa ni shujaa wa taifa lao. Inasimuliwa kuwa Mfame Daudi alikuwa ni kiongozi mdhalimu, fisadi, katili, mbakaji, mchawi, mwonevu na aliywatesa watu wa taifa lake. Hivyo, Fumo Liyongo anapambana kama shujaa kuliletea taifa hilo mabadiliko, jambo ambalo anafanikiwa kwa kusaidiwa na mkewe wa pili aliyeitwa Abanoye na mfuasi wake kindakindaki aliyeitwa Kibwana Mwengo Bashee. Aidha, kila juzu la hadithi na maudhui yake ambayo yanazungukia kisa hicho kikuu kinachomhusisha shujaa Fumo Liyongo na mfalme Daudi pamoja na mapambano baina yao.

Nadharia ya Mtengo

Utafiti huu umetumia Nadharia ya Mtengo iliyoasisiwa na Melvin Seeman mwaka 1959 na baadaye mwaka 1991 akaiboresha zaidi. Nadharia hii inaamini kuwa wahusika hupitia mitengo tofautitofauti ambayo huchochewa na mambo mbalimbali. Aidha, inaeleza kuwa mtengo mmoja unaweza kuibua, kujenga au kuathiri mtengo mwingine (Feuer, 1962; Faunce, 1981). Mtengo ni mionganoni mwa nadharia thabiti inayohusu masuala ya mitengo ya wahusika, kwani imefanikiwa kuunganisha nadharia nyingine na vipengele vingi vinavyounda na kuchanganua mitengo mbalimbali. Kutokana na hilo imekuwa ni faafu pia kwa utafiti huu, ambao unachambua vyanzo vinavyosababisha mitengo ya wahusika mashujaa ikiwemo ya kisaikolojia, kiutendaji na kijiografia kwa ujumla wake. Kwa hiyo, misingi mitano (5) ya nadharia hii imetumiwa na utafiti huu kufafanua vyanzo mbalimbali nya mitengo ya wahusika mashujaa. Misingi hiyo ni pamoja na:

- i. Usi-nafsiya: unahusika na hali ya kisaikolojia ya mhusika kujikana nafsi yake au kujichanisha na matakwa yake binafsi kwa nia fulani mahususi.
- ii. Udhafu wa kiutendaji: unarejelea uduni wa kimamlaka, kimaamuzi na kiutashi. Ni kitendo cha mhusika kukosa uwezo au kutoridhika na uwezo alionao katika kufanya maamuzi, kutawala, kudhibiti, kumiliki, kuongoza au kutenda mambo mbalimbali ambayo humlazimisha kujitenga au kutenga wengine kama njia ya kukabiliana na hali hiyo.
- iii. Uanomia: ni hali ya kukiuka, kuvunja au kuachana na kaida na taratibu zilizowekwa na kundi fulani, kisha kuunda na kufuata taratibu nyingine kwa lengo maalumu.
- iv. Umaanulizi: ni kitendo cha mhusika kushindwa kutambua maana ya kitu au jambo fulani, au kutoridhika na hali fulani. Mhusika hushindwa kuona maana ya hali fulani iliyopo au tija ya jambo fulani kutendeka, kiasi cha kutoridhishwa na mambo yalivyo na kukosa utulivu wa fikra, hivyo kuamua kutokubaliana/kujitenga nayo.
- v. Ukiushi wa kimila: unahusika na ukengeufu wa mila na miiko iliyowekwa na kundi au jamii fulani.

Kwa hiyo, misingi hiyo imeshirikiana kwa pamoja katika kufafanua vyanzo nya ujitekezaji wa mitengo mbalimbali ya kisaikolojia, kiutendaji na kimazingira ya mhusika shujaa katika utungo teule wa *Siri Sirini*.

Vyanzo nya Mitengo ya Wahusika Mashujaa katika *Siri Sirini*

Utafiti huu umebaini kuwa, mitengo mbalimbali ya kisaikolojia, kiutendaji na kimazingira ambayo huwatokea wahusika mashujaa huchochewa na vyanzo kadha wa kadha. Masuala yanayohusisha mazingira ya ndani ya kisaikolojia, tabia na nduni za wahusika, pamoja na mazingira ya nje ya kijamii, kiutamaduni na kisiasa, kwa pamoja yameshirikiana katika kuibua mitengo mbalimbali ya wahusika. Aidha, imeonekana kuwa chanzo fulani kinaweza kuibua mtengo zaidi ya mmoja kutegemeana na muktadha husika. Halikadhalika, imebainika kuwa, baadhi ya vyanzo vinavyoibua ama mitengo ya kisaikolojia au kiutendaji, kwa kiasi kikubwa pia vimeibua au kujengenya mitengo ya kimazingira. Hivyo, ujitekezaji wa mitengo mbalimbali ya kisaikolojia na kiutendaji, umeenda sambamba na ujitekezaji wa mitengo ya kimazingira kulingana na chanzo kilichohusika kuiibua mitengo hiyo. Kijumla, utafiti huu umebainisha vyanzo vitano (5) nya mitengo ya wahusika mashujaa katika utungo teule. Vyanzo hivyo ni pamoja na suala la hofu ya kiongozi kupinduliwa na shujaa, shujaa kutoridhishwa na utendaji wa kisiasa, mwito binafsi wa shujaa kitaifa, utanguzi wa miiko ya kimila na shujaa kukwepa uhasama wa kiakraba. Ufafanuzi wa namna vyanzo hivi vilivyoibua mitengo mbalimbali katika utungo wa *Siri Sirini* ni kama ifuatavyo:

Hofu ya Kiongozi Kupinduliwa na Shujaa

Baadhi ya wahusika katika kazi za kifasihi hususani viongozi wakuu, hujiona wamenyang'anywa uwezo, mamlaka na maamuzi kwa jamii zao kutokana na sifa anazokuwa nazo mhusika shujaa. Mara nyingi mhusika shujaa huwa na sifa za kipekee (zisizokuwa za kawaida na za uwezo wa juu kuwashinda watawala wao), hivyo viongozi husika hupatwa na hofu, kwani huwaona wahusika mashujaa kama tishio kwao na kulazimika kuwatenga. Kutokana na hofualiyonaoyo kiongozi, shujaa anakutana na mtengo, kwanza katika hali ya kisaikolojia kwani anawekewa mpaka wa kuhusiana na

kushirikiana na uongozi uliopo, kabla ya mtengo huo kudhihirika katika muktadha halisi kupitia vizuizi nya kicutendaji. Shujaa hukutwa na mitengo hii, si kwa sababu ya mambo halisi na ya kweli kwamba ni mwovu, ila ni kutokana na hofu ya kiongozi mkuu inayosababishwa na udhaifu anaokuwa nao dhidi ya sifa za kipekee za shujaa. Seeman (1959) anathibitisha hili kuwa, mtu anapokosa uwezo wa kufanya maamuzi au anapoijiona hana mamlaka na utashi wa kuzalisha matokeo yanayotarajiwa kutokea, moja kwa moja hujitenga au kumtenga mwgingine kama namna ya kijihami (Nadharia ya Mtengo). Aidha, Sarfraz (1997) anabainisha kwamba, si mara zote mhusika hukosa mamlaka au utashi, kwamba wakati mwgingine hudhani kuwa ameporwa uwezo na mamlaka yake, hata kama hali halisi haiko hivyo.

Suala hili limedhihirika katika *Siri Sirini* pindi tu masimulizi yanapoanza. Shujaa Liyongo anatengwa kisaikolojia na kicutendaji kutokana na hofu inayosababishwa na hali ya udhaifu wa kisiasa aliyonayo kiongozi wa taifa la Shanga ambaye ni Mfalme Daudi, kwamba anaweza kupinduliwa na kuporwa nafasi yake. Hali hiyo ya udhaifu aliyonayo ilitokana na ukubalifu wa Liyongo kwa watu wa taifa hilo, pamoja na haiba na uwezo wake mkubwa wa kiakili, kisiasa na kivita. Kutokana na hayo, ndipo Mfalme Daudi na uongozi wake wanajiona ni wadhaifu wakijilinganisha na Liyongo, kwa hiyo wanapatwa na hofu kwa kuhisi kwamba Liyongo anaweza kuwapindua katika nafasi zao. Madondoo yafuatayo yanathibitisha udhaifu wa Mfalme Daudi uliotokana na uwezo mkubwa wa Liyongo, uk. 4-5, I:

Mfano wa 1: Serikali ilikutimizia mahitaji na maslahi yako yote, lakini jinsi ulivyo haini, ultosheka wewe? La hasha! Ulitaka mwenyewe uwe mtawala mkuu...yaani wewe ndiwe Mfalme! *Ngurumo!* Ushahidi umo katika mashairi yako mwenyewe...nitakusomea...(*anasoma kisha anaendelea*) Sikilizeni: ni ajabu kuwa kiburi cha watu kama hawa kimewapelekea kujidanganya, wakidhami ya kwamba wao peke yao ndio walioelimika na ndio wajuzi wa mambo...mfungwa anasema yeye ni mzoefu wa mapambano...yeye huwaangamiza wote wenyenye kumkabili...huu ni uchochezi dhahiri jamani! Huyu mfungwa anatangaza kuingia kwenye bangu na kuangamiza wasio hatia ili yeye asonge mbele katika uongozi, akalie kitie cha enzi, kwa mabavu!....kejeli tupu!

Mahakamani, Hakimu anaendelea kutuliza watu, wale wanaoonekana kunong'ona na kuleta vurumai wanatupwa nje na askari, halafu anaendelea:

Mfano wa 2: Haya mfungwa unayejidai kusheheni weledi kuliko sisi sote wafafanulie wewe mwenyewe.....yaani mfalme anafananishwa na mbuzi....mbuzi huyo wa mwanamfaume amekamatwa pembe, yaani silaha zimedhibitiwa, na sasa Mfalme hawezu tena kujitetea.....yaani amedhibiti mali yake yote imara kabisa; na hivyo basi uwezo wake wa kuwakilisha wanawe, yaani sisi raia zake watiifu hana tena....Mfungwa amepambana na Mfalme wa haki na amemshinda. Sasa yeye mfungwa, ndiye amelinyakua jukumu la uongozi! Una la kusema mfungwa? (uk. 5-7, I)

Madondoo hapo juu yanaonesha namna viongozi walivyomwogopa Liyongo kwa kudhani kuwa anaweza kuipindua serikali na kuwa mfalme. Viongozi hao wanakiri kuwa Liyongo alikuwa na uwezo mkubwa kumzidi mfalme wao, hivyo wanayatasiri mashairi ya Liyongo kwamba alimfananisha mafalme na mbuzi na kumdhibiti kutokana na yeye kuwa na weledi zaidi yao. Vilevile, mashtaka yanaonesha namna uongozi mzima ulivyojiona ni mdhaifu kutokana na ustadi wa kiwango cha juu wa Liyongo katika vita. Wanakiri kwamba Liyongo alikuwa ni mjuzi wa mambo na mzoefu wa mapambano. Kwa hiyo uongozi wa Mfalme unajiona umekosa haki na mamlaka dhidi ya watu wao kwa kuzidiwa au kudhitibiwa na haiba na matendo ya jemedari huyo. Ni kutokana na hayo, Mfalme Daudi na viongozi wake wanamtenga shujaa Liyongo kisaikolojia na kicutendaji kwa kumwekeea mpaka asishiriki katika shughuli zote za kisiasa na wanamnyima haki ya kuwa huru na kuzungumza kwa kumweka kizuizini na baadaye kumfunga kifungo cha maisha, (uk. 4, 7-8: I):

Mfano wa 3:

“Kimya mahakamani! Mfungwa uliyesimama hapo unashakiwa kwa uhaini...utovu wa uzalendo...UCHOCHENI... Una la kusema mfungwa?”

“Ninalo” (*minong’ono ya chini kwa chini*)

“Hatuna muda huo unaotaka! Siku hizi zote tumekupa muda wa kutosha”

“Kifungoni?”

“Hata kama ni pangoni! Ulikuwa hai sio? Mbona hukujitayarisha vyema kwa utetezi? La, hasha! Mfungwa sinene!”

“Sasa nitajiteta vipi?”

“Nakwambia mfungwa sinene!”

“Kwa nini nisinene? Na toka hapo lini nikawa mfungwa? mlinitia mbaroni pasina sababu, mkanikweka korokoroni bila kujali haki zangu; sasa mmenileta kizimbani bila kutarajia kauli yangu! Wazee nini uamuzi wenu?” ...

“Mfungwa umepatikana na makosa yote uliyoshtakiwa kwayo...hukumu yako ni kuwa utafungwa maisha katika hali ya kinyama... na kama ukipanga njama huko huko ngomeni... basi huna budi kunyongwa hadi ufilie mbali kabisa!”

Katika dondo hilo, shujaa Liyongo anaitwa mfungwa bila hata ya kuhukumiwa. Mfalme Daudi na wafuasi wake wanaunda uzushi ambao unawasaidia kumshitaki na kumtenga kama mbinu ya kuendelea kujihami na kulinda nafasi zao za uongozi. Kwa hiyo kupitia uzushi huo, viongozi na mahakama wanafanikiwa kumsababishia Liyongo mtengo wa kisaikolojia na kiutendaji, pale wanapomshitaki kama mchochezi, mtovu wa uzalendo, mhaini na mwalifu kwamba alitaka kumpindua Mfalme kupitia mashairi yake. Hii ilitosha kudhihirisha kuwa tayari uongozi wa Mfalme Daudi ulikwishadhamiria kumtenga shujaa Liyongo, ili asijihuise tena na masuala ya kisiasa chini ya uongozi wao. Aidha, Liyongo anapokuwa kizimbani, mahakimu na wazee wa mahakama wanamnyima haki ya kujitetea na wanamweka kizuijini kwa kumfunga kifungo kisicho cha haki.

Hivyo kupitia hayo, shujaa Liyongo anakutana na mtengo wa kisaikolojia na kiutendaji, kwani anakosa fursa ya kuendelea kuhusiana na kuingiliana; si tu na utawala wa Mfalme Daudi, ila pia na wanajamii wa taifa la Shanga, ambao wengi walimkubali na kumpenda kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuwatetea na kupigania haki zao. Kwa hiyo, shujaa Liyongo anatengwa kisaikolojia na kiutendaji pale anapowekewa mpaka au anapozuiwa asijihuise na masuala ya kisiasa, pia anakutana na mtengo wa kizuijini, ambao unakamilika pale anapofungwa kifungo cha maisha.

Shujaa Kutoridhishwa na Uongozi Uliopo

Chanzo kingine cha mitengo ya wahusika mashujaa ni suala la shujaa kutoridhishwa na utawala wa kisiasa uliopo. Tofauti na ilivyokuwa kwa shujaa kutengwa na kiongozi mkuu, hapa shujaa ndiye hujitenga mwenyewe kutokana na masuala ya kisiasa yanayoendelea. Suala la mhusika kutoridhishwa na jambo fulani limedokezwa na Seeman (1959) kama hali ya umaanulizi kwamba huanzia katika saikolojia ya mhusika. Seeman (*keshatajwa*) anaeleza kuwa, mhusika hujitenga pale anaposhindwa kuona maana ya hali fulani iliyopo au tija ya jambo fulani kuendelea kutendeka, kiasi cha kutoridhishwa na mambo yalivyo na kukosa utulivu wa kifikra.

Nao Almond & Verba (1965), House & wenzake (1985), Finifter (1970) na Wood (2014) wanaeleza hali hiyo kupitia mitengo ya kisiasa. Maandiko yao yanakubaliana kuwa, mifumo ya kisiasa iliyopo husababisha watu kupoteza imani dhidi ya viongozi na kuwafanya wasiridhishwe kiasi cha kuamua kujitenga nayo. Finifter (1970:390) anaendelea kuthibitisha hili anaposema “*hali hii ya mtengo hujidhihirisha pale mhusika anaposhindwa kutambua maana ya vitendo vya kisiasa vinavyoendelea, kwamba vitendo hivyo havina maana kutokana na kwamba haviwezi kuleta matokeo yoyote chanya, havitumiki kubadilisha hali ya jamii*” (tafsiri yangu). Hali hii ni dhahiri katika Siri Sirini, kwani zimemchochea shujaa husika (Liyongo) kujitenga kwa kupinga kaida za kisiasa zilizopo, kutokana na kwamba zinawakandamiza wanajamii.

Katika Siri Sirini, shujaa Liyongo anaonesha kutoridhishwa na utendaji wa kisiasa wa Mfalme Daudi na anakosa imani nao, kiasi cha kuamua kuijweka mbali na mfumo mzima wa kisiasa kisaikolojia, kiutendaji na hata kimazingira. Hii ilisababishwa na mfalme huyo kuwa mdhalimu na mwovu. Mwandishi anaeleza kuwa Mfalme Daudi alidhulumu na kuwaonea watu, alipora mali za wanyonge na alitumia rasilimali za jamii kwa manufaa yake binafsi. Kutokana na maovu hayo, shujaa Liyongo anaona kwamba uongozi wa Mfalme Daudi hauna maana kwa kuwa hauinufaishi jamii yake. Hivyo, Liyongo anajitenga kisaikolojia na kiutendaji kwa kukiuka propaganda na itikadi za kisiasa zilizopo. Liyongo haungi mkono shughuli za kisiasa na anaupinga waziwazi uongozi wa Mfalme Daudi, kwa kubainisha upande alipo, uk. wa 198, III anasema:

Mfano wa 4: “Nakubali. Mimi naunga mkono wale wenye kutaka mabadiliko kamili, sio nusu nusu... Tena nasema hakuna mwiya wa kulimati, tukilaza damu, kwa sababu Daudi Mringwari na tasa wake wa nadharia waliosambaa kote kote saa hizi, wanajizatiti kwa mapambano makali... pendekezo ni lile lile tuliloafikiana...”

Dondoo hili linaonesha namna Liyongo alivyoomua kuachana na kupingana na uongozi uliokuwepo kutokana na mfumo mzima wa kidhalimu uliokuwepo. Katika mazungumzo baina ya Liyongo na wafuasi wake, Liyongo anajipambanua waziwazi kuwa ameamua kuungana na wale wanaotaka mabadiliko, na si mabadiliko tu, ila mabadiliko kamili; yaani wale walioomua kwa gharama yoyote kupigania ukombozi wa Washanga. Liyongo anawachochea wafuasi wake kuwa wanapaswa kuwa tayari, na kuanza haraka harakati zao kwa kuunda jeshi ili kipingana na Mfalme Daudi na wenzake wenye mitazamo tasa isiyozaa matunda au kuwa na faida yoyote kwa jamii.

Halikadhalika, Liyongo anaonesha namna asivyordhishwa wala kukubaliana na shughuli za kisiasa za kikandamizaji pale alipoamua kuihama nchi ya Shanga na kwenda Ozi. Shujaa Liyongo kutokana na kutoridhishwa na siasa za Mfalme Daudi kiasi cha kukosa tena imani nazo, anachukua maamuzi ya kujitenga nazo kimazingira kuititia mtengo wa uhamishoni. Suleiman Mringwari (mtoto wa Mfalme Daudi) katika kikao, anaonesha namna Liyongo alivyopingana na serikali yake hadi kufikia hatua ya kuihama nchi kwa sababu ya kutoridhishwa na kukosa imani nayo, (uk. 207: I):

Mfano wa 5: Mimi nafikiri la kufanya, bila kuchelewa, ni kumtafuta Fumoloti na kujaribu tena kupalilia imani baina yetu na yeye. Kukosekana imani kati ya pande hizi mbili ndiko kulikosababisha mtibuko huu. Mringwari alidai. Watu wazima wote walimwangazia macho visivyo.

Katika dondo hilo, maoni anayoyatoa Suleiman Mringwari katika kikao, yanaonesha namna Liyongo alivyokosa imani kwa uongozi uliokuwepo kiasi cha kuamua kuihama nchi. Suleiman anakiri kuwa, kukosekana kwa imani ndiko kulikoibua mtafaruko huo uliosababisha Liyongo atoroke na kuhamia katika nchi ya Ozi, ili kutumia fursa hiyo kupanga mikakati ya kuikomboa nchi yake. Kutokana na hilo, Suleiman anamshauri Mfalme na viongozi wake kwamba wamtafute Liyongo na waijenge imani iliyovunjika baina yao. Hivyo, kuititia mtengo huu Liyongo anajiveka mbali na mfumo wa kidhalimu wa Shanga, yaani anapingga siasa za Mfalme Daudi na wafuasi wake. Shujaa Liyongo hashirikiani nao wala kuunga mkono masuala ya kisiasa yanayoendelea kwani aanaona hayana maana yoyote kwa kuwa hayaisaidii jamii ila zaidi yanawanyima haki zao. Vilevile, shujaa Liyongo anaihama Shanga (mtengo wa uhamishoni), ili kupanga mipango ya kuikomboa jamii yake, jambo ambalo lilimsaidia kufanikisha jaala yake ya msako wa mabadiliko ya nchi Shanga.

Mwito Binafsi wa Shujaa Kitaifa

Mwito ni hali ya kuita au kuitwa; ni agizo rasmi la kutekeleza jambo (TUKI, 2014; BAKITA, 2016). Kwa hiyo, mwito binafsi wa shujaa kitaifa unahusisha msukumo na agizo binafsi la ndani la shujaa kujitoa mhanga ili kutekeleza masuala muhimu ya kimajumui kwa manufaa ya taifa lake. Katika tungo za kitendi, mhusika shujaa huamini kuwa ameitwa na umma; anahitajika zaidi na wanajamii kuliko kuhangaikia maisha yake binafsi, hivyo mapambano yake hulenga kuinufaisha jamii. Shujaa hapigani peke yake au kwa maslahi yake binafsi; hupigana pamoja na, na kwa ajili ya, kundi lake analoliwakilisha na analolitetea. Kundi hili huweza kuwa kijiji, jamii fulani, kikosi, kabilia au hata

taifa (Mulokozi, 1999:12). Kwa hiyo kwa kiasi kikubwa, rajua na malengo ya shujaa katika kuishi kwake huwa ni yale yaliyo na tija kwa taifa lake kuliko kwake binafsi. Hivyo hukubali kujitoa chambo na kwa gharama yoyote, ilimradi kufanikisha matakwa muhimu ya kijamii. Matakwa muhimu ya kijamii yanajumuisha mambo yote yenyewe kustawisha jamii kama vile utu, haki, usawa, amani, maendeleo ya vitu, huduma bora za kijamii kwa watu wote, uongozi bora na kadhalika. Mwito binafsi alionao shujaa katika kuipigania jamii na taifa lake ni chanzo muhimu cha mtengo hasa wa kinafsi/kisaikolojia anaokutana nao mhusika huyu. Ufafanuzi wake unadhihirika zaidi katika maandiko yanayoeleza kuhusu dhana ya ushujaa na shujaa (Knappert, 1983; Johnson, 1986; Okpewho, 1979; Mulokozi 2002, 2017; Sosoo, 2018).

Katika *Siri Sirini*, shujaa Fumo Liyongo anajitenga na masuala yake binafsi kutokana na mwito wa ndani aliokuwa nao kwa ajili ya kupigania mabadiliko ya kijamii. Liyongo alikuwa na nia ya dhati katika kutumikia taifa lake la Shanga, na alikuwa tayari kutoa maisha yake yote kama sehemu ya kuwatumikia wanajamii. Kujitoa huko kwa Liyongo kulichochewa na mambo ya kidhalimu na uonevu uliokuwa ukifanywa na Mfalme Daudi na viongozi wenzake kwa jamii yake. Ni kutokana na uongozi mbaya wa Mfalme Daudi, ndipo shujaa Liyongo anawiwa kuiacha familia yake na kwenda mafichoni, halikadhalika kuiacha tena familia yake mpya ya huko mafichoni ili kuendeleza mapambano ya kuikomboa jamii yake. Katika ukurasa wa 77-78: III, tunaona Liyongo anavyokiri kwa ndugu yake Mwanamfaume (mtoto wa Mfalme) kuwa yeche kurudi nyumbani ni thama mahususi na si suala la uteuzi, mwandishi anasema:

Mfano wa 6: Kimoyomoyo alijuua asiporudi Shanga nchi hiyo itaingia katika hatari kubwa...Hapohapo akaamua kurudi kwao ili akajishughulisse kikamilifu katika kuyarekebisha mambo. "Nimekubali kurudi nyumbani". Kaa ana kwinginepo wapi ila kwenye lakwe gando?". Kwangu mie kurudi nyumbani si swala la uteuzi, bali ndio wajibu haswa! Thama mahususi!

Nukuu hii inabainisha jinsi ambavyo familia haikuwa kipaumbele kwa Liyongo ikilinganishwa na taifa lake, hivyo anajitenga nayo kwa kusudi la kuipigania nchi yake. Liyongo aliamini kuwa hapa duniani alikuwa na jukumu moja tu la msingi la kuiletea Shanga mabadiliko. Sambamba na hilo, Kibwana aliyeokuwa mfuasi wa Liyongo anaonesha namna Liyongo alivyojitenga na masuala yake kibinafsi na kujishughulisha zaidi na mambo ya kijamii kwa kuwa mstari wa mbele katika mapambano ya kupigania mabadiliko ya jamii yake, ukurasa wa 308: III Kibwana anasema:

Mfano wa 7: Sote twakubaliana kuwa Fumo Liyongo wa Bauri...Fumoloti, simba buka wa Shanga na Ozi, ndiye haswa aliyetukombo...Fumo Liyongo hakujifikiria yeche mwenyewe alipojitolea kikamilifu na kupiga mbizi, kichwa mbele, katika ngama ngumu ya mapambano...alipiga mbizi nchi kavu kwa mapenzi yake mwenyewe huku akijua matokeo yake ni kufa au kupona.

Nukuu hiyo inathihirisha namna ambavyo Liyongo alijitenga na masuala yake binafsi na kujishughulisha na mambo ya kijamii siku zote za maisha yake. Shujaa Liyongo ndiye mtu pekee aliye kubali kujikana kufa na kupona ili kutetea maslahi mapana ya jamii. Aidha, harakati na msukumo huo binafsi wa Liyongo ambaa aliona anapaswa kuutekeleza kwa taifa lake, ndio uliomsukuma Liyongo kumjuza mke wake wa pili wa nchi ya ugenini (Abanoye) hamu yake ya kutaka kurejea nyumbani ili kuendeleza mapambano ya kupigania haki za wanajamii wenzake zilizopotea kwa muda mrefu. Katika ukurasa wa 104:III mwandishi anaonesha mtengo wa Liyongo dhidi ya nafsi yake mwenyewe, uliochochewa na jukumu mahususi kwa taifa lake; anasema Liyongo "aliikuwa na hamu kubwa; hamu ya kutekeleza jukumu lake mahususi maishani. Huo aliuona ni wajibu wake kwake yeche mwenyewe binafsi, na kwa Washanga wengine wote ambaa hawajapata fursa ya kustaladhi kitu haki". Hivyo wajibu huo, ndio unaokuwa mwito wake wa asili na kumsukuma hadi kumwaga mkewe kipenzi na kujitenga na familia yake mpya ili kurejea Shanga.

Kwa ujumla, shujaa yejote wa tungo za kitendi, analo jukumu binafsi la kuitumikia jamii yake kwa nia ya kuikomboa dhidi ya udhalimu na mambo mengine maovu. Kwa shujaa yejote, kujitenga kisaikolojia na masuala yake binafsi na kushughulika na masuala ya kijamii kwake ni faida, na familia

kwake si kipaumbele sana. Kwa hiyo, maisha na matendo yake hubakia kuwa faida kwa jamii, na aghalabu mhusika shujaa huendelea kuishi/kukumbukwa katika jamii hata baada ya baada ya kifo chake.

Shujaa Kukwepa Uhassama wa Kiakraba

Uhassama ni hali ya kufarakana kutokana na ugomvi, uadui, wivu au chuki (TUKI, 2012; BAKITA, 2016). Aidha, neno ‘akraba’ linarejelea mtu wa familia moja, yaani ndugu au jamaa wa karibu wa ukoo mmoja (TUKI, 2019). Katika *Siri Sirini*, uhassama kati ya akraba wawili wa kiume wa aila/ukoo mmoja unaibuka, kwa sababu ya husuda ya mtoto wa mjomba (Mfalme Daudi) dhidi ya jamaa yake ambaye ni mtoto wa shangazi yake (Fumo Liyongo). Shujaa Liyongo wa Bauri (mtoto wa shangazi wa Mfalme Daudi) anaonewa kijicho na akraba yake, Mfalme Daudi (ambaye ni mtoto wa mjomba wa Liyongo) kwa sababu ya haiba, zihii na urazini wa kiwango cha juu alionao. Mambo hayo yanafanya Mfalme Daudi kumwonea wivu Liyongo kutokana na uwezo wake. Kadhalika hofu, chuki na uadui zinaonekana kumzidi Mfalme Daudi, pale anapogundua kuwa Liyongo anapendwa na kukubalika sana na watu. Hali hiyo inamfanya Liyongo kuwa mshindani na mpinzani wa Mfalme katika taifa zima la Shanga. Uhassama kati ya Liyongo na Mfalme Daudi unathibitika kuititia mazungumzo ya Liyongo na mkewe wa pili Abanoye. Liyongo anamsimulia Abanoye mambo hayo katika ukurasa wa 47: III, kwamba:

Mfano wa 8: Ilianza kubainika, tangu mwanzo kwamba mimi, sio Daudi, ndiye niliyekuwa na nadharia angavu, ruwaza wazi, urasimu rasmi, haiba ya kifalme na urazini mweledi! Ni maumbile yangu tu ndiyo yaliyomtatanisha na kumbabaisha Daudi...Mathalani, nilikuwa mrefu kumshinda, tena kwa mbali basi siku hizo. Labda alijilinganisha nami, akajiona mtu mfupi sana asiyevutia, sijui!...nilikuwa mnyenyeketu sana, ilivyosemekana mwingi wa neema iliyanusurika na kututumka kutoka katika kiini cha kati cha maumbile yangu. Si tu katika majibizano, nilikuwa na usahili uliowapendeza sana waungwana na kuwavutia kwangu kama smaku vile... “Yote haya bila shaka hayakumpendeza mkoi wako?” (*aliuliza Abanoye*)... “Shabash!” *alikuli Liyongo*...Uadui ukaanza, kuanzia hapo Daudi daima akawa mtu wa kufura, kunung’unika, kununa na kulia ngoa! Hakuionja bashasha tena! Chini kwa chini chuki ikawa inavukuta kama tanuri! Hadi leo hajanisamehe bado.

Dondoo hapo juu linaonesha kwamba, haiba bora ya kitabia, kiakili na kimaumbile aliyojaaliwa shujaa Liyongo ndizo zinamfanya ndugu yake Daudi kumchukia na kumwonea wivu. Hivyo, ili kuepukana na ugomvi ambaa ungeweza kusababisha vita kubwa baina ya akraba hao wawili, ndipo Liyongo anakutwa na mtengo wa uhamishoni. Data ifuatayo uk. 48-49 inathibitisha haya:

Mfano wa 9:

Mara tu alipokikalia kiti cha enzi matako mawili kisawasawa, Mfalme Daudi Mringwari alionesa uhassama dhihi yangu na hata shangazile, aliyemlaumu waziwazi ati kwa kunipendelea mimi mwanawe!

Abanoye: Bi Mwanaziza akafanye?

Liyongo: Afanyeje na mwenye nguvu ni mwingine?! Siku hizi zote aliushuhudia barabara sana mtafaruku huo wa fahali zake wawili. Alipoona hali imepindukia daraja yake ya hatari, akaamua amuondoe mmoja ilimradi ampatie nafasi tosha huyo mwingine atawale zizi lake gisi apendavyo!

Abanoye: Aliywondoa zizi la Shanga alimpeleka zizi gani?

Liyongo: Zizi la Manga. Kuko huko! Hakuwa na hiari sini! Tukaishi huko kwa muda wa miaka mitano mizima! Tukarudi Shanga nilipokuwa barobaro shababi, damu ikiniforeka mishipani kama nini sijui; nimetutumka ungedhani nitaripuka.

Kwa kurejelea data hapo juu, shujaa Liyongo akiwa na miaka kumi na mitano anaihama nchi yake kwa miaka mitano (mtengo wa uhamishoni) akisaidiwa na mamaye, ili kuepuka kugombana na

nduguye. Hivyo, Liyongo na mama yake wanaondoka Shanga na kwenda kuishi uhamishomi katika nchi ya Manga ili kuepusha uhasama huo ulioanza kuibuka.

Utanguzi wa Miiko ya Kimila

Mara nyingi utabiri na uajabuajabu unaoambatana na kuzaliwa kwa shujaa huwa ni taashira kuhusu upkee wa mtoto huyo. Taashira ni ishara, dalili au hali inayoshiria jambo fulani. Katika muktadha wa kifasihi, ishara huchukuliwa kama jazanda inayobeba dhana nyingine ndani yake. Wazo kuwa taashira ni ishara inayoweza kuchukuliwa kama jazanda ya jambo au kitu kingine linawekwa bayana na Mulokozi (2017:167) anapoeleza kuwa, ishara ni upeo wa sitiari. Katika ishara, kitu fulani kinachofahamika au kuaminiwa na jamii fulani hutumika kuwa alama ya kitu kingine na huelewaka hivyo kwa wanajamii wengi. Mulokozi (*keshatajwa*) anaendelea kueleza kuwa ishara nyingi huwa ni jumui za kimapokeo; kwamba huaminiwa na jamii yote na hurithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Halikadhalika kwenye tungo nyingi za kitendi, ishara/matukio yanayotokeza kabla au wakati wa kuzaliwa mhusika shujaa, huaminiwa na wahusika wanajamii kwamba yanaashiria jambo fulani wakiyahusisha na mila na falsafa zao. Hata hivyo, matukio mengi yanayotokea wakati wa shujaa kuzaliwa, mara nyingi huwa ni mwiko kulingana na utamaduni wa wanajamii husika.

Mwiko ni mambo ambayo ni marufuku, yasiyoruhusiwa kutokea kwenye jamii kwa mujibu wa imani, mazoea, utamaduni na desturi za jamii husika, kwani yanapotokea huamini yanaashiria au kuleta majanga kwenye jamii husika. Kutokana na kuzaliwa kwa shujaa kuambatana na matukio/taashira ambazo ni za kimiiko, wanajamii huamini kuwa mtoto aliyezaliwa anaashiria balaa, hivyo huchukuliwa ametangua/ amevunja miiko ya kijamii. Taashira hizo huwa ni za kiajabuajabu/ kimuujiza/ kinduni yaani huwa si za kawaida kwa kuwa haziwezi kutokea katika mazingira ya kawaida. Kwa hiyo uajabuajabu huo huaminiwa na wanajamii kuwa mtoto anayezaliwa katika mazingira hayo huwa ni kioja, mkosi, janga au tishio kulingana na imani na utamaduni wa jamii husika.

Seeman (1959) anaeleza kwamba, mtu anapoasi au kukiuka mila na tamaduni zilizoasisiwa, kuaminiwa na kukubaliwa na jamii nzima, hujitenga yeye mwenyewe, na hatimaye kumsababishia mhusika huyo pia mtengo wa kijamii. Sarfraz (1997:56) akimnukuu Funce (1981:135) anathabitisha suala la mtengo mmoja kuibua mwingine anaposema “*although these all variants of alienation seem conceptually independent of one another but actually they are inter-related to one or the other way, they may form a casual chain in which one or more types of alienation tend to produce another*”. Kwa tafsiri yetu, Sarfraz anasema, “japokuwa vijenzi vyote vya mtengo vinaonekana kujitegemea, vinaingiliana kwa namna moja au nyingine, vinaweza kutengeneza muingiliano kwamba, aina moja au zaidi ikajenga/ikaibua nyingine”. Kutokana na maelezo ya Sarfraz (1997), mhusika anaweza kujitenga kimila na kusababisha vilevile jamii nzima kumkataa, aidha kumuengua kisaikolojia au kijiografia kutokana na ukiukwaji wa desturi zao. Kwa hiyo shujaa anapovunja miiko hiyo anakutwa na mitengo miwili. Kwanza kisaikolojia kuvuka mpaka wa kihulka na kisifa yeye mwenyewe bila kujua kutokana na matukio ya kinduni yanayomzunguka, pili, wanajamii kumkataa kisaikolojia na kijiografia. Kwa hiyo, kuvunjwa kwa masuala kama haya ambayo kiutamaduni huwa ni mwiko ni mionganoni mwa chanzo cha mitengo ya wahusika mashujaa.

Katika utungo wa *Siri Sirini*, Liyongo kuvunja miiko ya kimila kulikosababishwa na matukio ya kiajabu yaliyoambatana na kuzaliwa kwake, kisaikolojia kunatengeneza mpaka dhidi ya jamii yake akiwa mtoto mdogo. Tunaambiwa kuwa Bi. Mwanaziza (mama wa Liyongo) alikaa na mimba ya Liyongo kwa takribani miezi kumi na miwili kabla ya kumzaa. Pia baada ya kuzaliwa kwake, alianza kuongea, na alizaliwa akiwa na meno tayari. Kutokana na matukio haya moja kwa moja kisaikolojia Liyongo alijiweka mbali na jamii yake kutokana na sifa zisizo za kawaida alizokuwa nazo, kwani alijipambanua kuwa si mtu wa kawaida tena. Matukio haya yalikuwa ni mwiko kutokea katika jamii yao, na yalipotokea mtoto alipaswa kuuawa, kwa kuwa waliamini ni kituko na balaa katika jamii. Suala hili lilimfanya Liyongo pia atengwe na wanajamii kwani walimkataa na kutaka kumuua kwa kuogopa kushirikiana naye. Katika ukurasa wa 42-43: III, masimulizi ya Liyongo kwa mkewe Abanoye yanaonesha hayo kama yanavyodondolewa hapa chini:

Mfano wa 10: Mtoto huyo hakuzawa mwezi huo bali miezi miwili mitatu baadaye...tokea hapo, si uvumi huo? Baadhi ya watu walidai ya kwamba mtoto alizaliwa na meno yake tayari...na si hayo pekee...kuwa badala ya kilio cha mwana kurasua hewa, mtoto tayari alisema maneno...tena ya kiutuuzima! Si uzushi hunu... Wengi waliodai kwamba walishuhudia yote hayo walitaka auwe, lakini wazazi wakawayi kumnusuru. Hima walimhamishia Pate. Mpaka pale mtoto alipokuwa na umri wa miaka saba, na kama isemekavyo, tayari akiwa na kimo cha takriban mtu mzima. (*Abanoye*) Ndipo waliporudi Shanga? (*Liyongo akakuli*) Sadakta. (*Abanoye*) Mara hii Washanga hawakutaka kumfishaa lakini? (*Liyongo*) Hawakulifiria kamwe hilo! Labda walikuwa washasahau kuwa hicho kivulana kirefu ni yule yule kigego!

Kwa mujibu wa mila na desturi za watu wa taifa la Shanga, hali ya mtoto kupitiliza miezi ya kuzaliwa ilikuwa ni utabiri tosha kwamba mtoto atakayezaliwa si wa kawaada, na moja kwa moja alikuwa ameasi, kwamba amejitenga yeye mwenyewe kwa kukiuka mwenendo wa kitamaduni wa jamii yao. Halikadhalika, mtoto Liyongo alitengwa kisaikolojia kwa kukataliwa kuhusiana na jamii nzima na kimazingira pale walipotaka kumuua. Kwa ujumla, shujaa Liyongo alijitenga mwenyewe kisaikolojia bila ya kujua baada ya kuzaliwa kwake kuambatana na hali za kiajabu, alitengwa na jamii yake pale ilipoweka mpaka wa kuhsiana naye pindi tu alipozaliwa. Halikadhalika, mitengo hiyo ilimsababishia shujaa mtengo mwengine wa kimazingira ambaa ni mtengo wa uhamishoni, kwani ilimbidi kuhamishwa na mama yake kutokana na mtengo huo wa kijamii uliokuwa umemkuta. Kwa ujumla, inapotokea mtoto akazaliwa na matukio kama hayo, wanajamii huamini kuwa ni ishara ya kutokea kwa balaa au majanga kwenye jamii yao. Shujaa huonekana kioja na moja kwa moja kidesturi huwa ameasi (amejitenga kiutamaduni) na kusababisha kukataliwa (kutengwa kijamii) na jamii yote.

Hitimisho

Kwa ujumla, makala hii imeeleza vyanzo mbalimbali vya mitengo ambavyo vinahusisha masuala ya kisaikolojia, kijamii, kisiasa na kiutamaduni Suala la shujaa kuwa tishio kwa kiongozi mkuu, shujaa kutoridhishwa na uongozi uliopo, mwito binafsi wa shujaa, utangizi wa miiko ya kimila na shujaa kukwepa uhasama wa kiakraba ni mionganoni mwa vyano vilivyoonekana kuibua mitengo mbalimbali ya wahusika mashujaa. Makala hii inaona kuwa, kutokana na vyanzo hivi kuwa ni mahuluti, kwa kiasi kikubwa huibua mtengo zaidi ya mmoja, pale mtengo mmoja unapoibua au kujenga mwengine. Hivyo, vyanzo/ mambo hayo ndiyo yaliyoibua mitengo ya kisaikolojia, kiutendaji na kimazingira. Hata hivyo, utafiti zaidi unapaswa kuendelea kuhsiana na kipengele cha mitengo ya wahusika. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa tafiti za kiulinganishi, pia kuchunguza mchango wake kwa wahuska mashujaa na kwa jamii zao kwa ujumla wake.

Marejeleo

- Ansari, M. S. (2013). "A Study of the Themes of Alienation, Detachment and Relationship Crises in Anita Desai's Major Novels". *Language in India*, 13(5), 566-581.
- BAKITA (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Campbell, J. (1956). *The Hero with a Thousand Faces*. New York: Meridian Books.
- Chiduo, E. F. K., Chimerah, R., Kaoneka, M., Yahya, R., & Attas, A. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. Nairobi: English Press Ltd.
- Chimerah, R. M. (2013). *Siri Sirini: Mshairi na Mfungwa*. Kitabu cha 1. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.
- Chimerah, R. M. (2014). *Siri Sirini: Mpiga Mbizi Kilinini*. Kitabu cha 2. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.
- Chimerah, R. M. (2014). *Siri Sirini: Mtihani wa Mwanamke*. Kitabu cha 3. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.
- De Vries, J. P. N. (1963). *Heroic Song and Heroic Legend*. London: Oxford University Press.
- Durkheim, E. (1976). "Anomie and Suicide". Katika L. A. Coser, & B. Rosenberg (Wah.), *Sociological Theory* (kur. 415-424). New York: Macmillan.
- Einblau, D (1965). "Alienation a Social Process". M.A Thesis. University of Alberta.
- Faunce, W. A. (1981). *Problems of an Industrial Society*. New York: McGraw-Hill.

- Feuer, L. (1962). "What is Alienation? The Career of a Concept". *New Politics*, 1, 670-677.
- Gathara, F. (2013). "Taswira ya Jagina katika Tendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa". Tasinifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Gichamba, J. M. (2005). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu Wao katika Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu". Tasinifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Hegel, G. W. F. (1949). *Phenomenology of Mind*. J. B. Baillie (Mtaf.). NY: Macmillan.
- Kluckhohn, C. (1959). Recurrent Themes in Myths and Mythmaking. *Daedalus*, 88(2), 268-279.
- Merton, R. K. (1957). *Social Theory and Social Structure*. Glencoe, Illinois: Free Press.
- Michaux, G. (2003). *Gilgamesh and Homer: A Comparative Study of Motifs Sets, Distinctions and Similarities*. Tasinifu ya Umahiri. (Haijachapishwa). Antwerpen: Open Universitet.
- Mulokozi, M. M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatuzza Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: MNP.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasibi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mwangi, J. N., Nabea, W., & Wandera, S. (2019). "Ulinganishi wa Matatizo ya Kijamii Yanayowakumba Majagina katika Tendi za Mikidadi na Mayasa na Kalerala". *Kiswahili*, 1(1), 14-21.
- Ndalu, A. E., Babusa, H. & Mirikau, S. A. (2013). *Kamus Teule ya Kiswahili: Kilele cha Lugha*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Nyamsenda, J. C. (2015). "Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari". Tasinifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Propp, V. (1968). *Morphology of the Folktale*. Indianapolis: American Folktale Society and Indiana University.
- Raglan, L. (1956). *The Hero*. New York: American Library.
- Rank, O. (1909). *The Myth of the Birth of the Hero: A Psychological Exploration of Myth*. (Exp. & updated ed.) (G. C. Richter & E. J. Lieberman, Wataf.). London: The Johns Hopkins University Press.
- Rousseau, J. (1947). "The Social Contract". Katika E. Barker (Mh.), *Social Contract* (kur. 237-440). London: Oxford University Press.
- Sarfraz, H. (1997). "Alienation: A Theoretical Overview". *Pakistan Journal of Psychological Research*, 12(1-2), 45-60.
- Seeman, M. (1959). "On the Meaning of Alienation". *American Sociological Review*, 24(6), 783-791.
- Seeman, M. (1991). "Alienation and Anomie". Katika J. P. Robinson & P. R. Shaver (Wah.) *In Measures of Personality and Social Psychological Attitudes*. (kur. 291-371). San Diego, CA: Academic Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (1997). "The Significance of the Journey in Folktales from Zanzibar". Tasinifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Shah, M. I. (2015). "Marx's Concept of Alienation and its Impacts on Human Life". *Al-Hikmat*, 35, 43-54. <http://www.pu.edu.pk/home/journal/11>
- Sosoo, K. F (2018). "Ushujaa katika Motifu ya Safari na Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania". Tasinifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- TUKI. (2006). *Kamus ya Kiingereza- Kiswahili*. Toleo la Tatoo. Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI. (2014). *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Tatoo. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI. (2019). *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Nne. Nairobi: Oxford University Press.

